Ofisi ya Rais
Sekretarieti ya Ajira
katika Utumishi wa Umma

# AJIRA MAGAZINE

Toleo Na. 3, 2026

# Katibu Kiliba awaaga Sekretarieti ya Ajira baada ya kustaafu.

*“Leo hii nawaaga nikijivunia ushirikiano wenu mkubwa mlionipa katika kipindi chote nilichokuwa hapa, niwaombe sana muendelee kufanya kazi kwa bidii na uzalendo ili kuhakikisha taifa letu linapata watumishi bora" Kiliba*




Septemba 2026



Matokeo ya Usaili wa Mahojiano sasa yawekwa wazi

Ajira Portal yaja na maboresho mapya kwa waombaji ajira

# Katibu Kiliba awaaga Sekretarieti ya Ajira baada ya kustaafu

Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Mick Kiliba amesema kuwa amejivunia umoja na mshikamano ambao umekuwepo katika taasisi hiyo kwa kipindi chote ambacho amefanya kazi.

Bw. Kiliba aliyasema hayo alipokuwa akiwaaga viongozi na watumishi wa Sekretarieti ya Ajira baada ya kustaafu katika Utumishi wa Umma.

Bw. Kiliba amesema anastaafu Utumishi wa Umma akiwa na furaha kwa namna alivyofanya kazi na watumishi wenzake kwa umoja na mshikamano na kutanguliza maslahi ya taifa mbele katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za taasisi ikiwemo uendeshaji mchakato wa ajira.



"Leo hii nawaaga nikijivunia ushirikiano wenu mkubwa mlionipa katika kipindi chote nilichokuwa hapa, niwaombe sana muendelee kufanya kazi kwa bidii na uzalendo ili kuhakikisha taifa letu linapata watumishi bora" alisema.





# USAILI WA MAHOJIANO





## Matokeo ya Usaili wa Mahojiano sasa yawekwa wazi

Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imefanya maboresho katika mfumo wa Ajira Portal kuwezesha upatikanaji wa taarifa za matokeo ya usaili wa mahojiano ya ana kwa ana (Oral interview.)

Wale waliofaulu na kuhifadhiwa kwenye Kanzidata wamepata status za “Passed and stored into Databank”

Wasailiwa ambao hawakufaulu usaili wamepata ujumbe wa “Scored below average passmark”.


Wote ambao wako kwenye Kanzidata na wasipopata ajira baada ya muda wa mwaka mmoja watapata ujumbe wa “databank has been expired

# Sekretarieti ya Ajira yaanzisha Huduma ya Live Chat Kupitia Ajira Portal

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imekuja na huduma mpya ya Live Chat kupitia Ajira Portal, inayolenga kurahisisha mawasiliano kati ya waombaji wa ajira na watoa huduma wa Dawati la Huduma kwa Wateja.


Kupitia huduma hiyo, muombaji wa ajira anaweza kuwasiliana moja kwa moja na mtoa huduma kwa njia ya kuchati, kuuliza maswali mbalimbali na kupata majibu kwa wakati. Huduma hiyo pia inamwezesha mtumiaji kujipatia msaada na kujihudumia mwenyewe kupitia mfumo wa Ajira Portal.

Uanzishwaji wa huduma ya Live Chat ni miongoni mwa hatua zinazochukuliwa na Sekretarieti ya Ajira katika kuondoa changamoto zinazowakabili waombaji wa ajira na kurahisisha upatikanaji wa huduma, msaada na taarifa muhimu katika hatua mbalimbali za mchakato wa ajira.




## Lengo la huduma ya Livechat

Huduma hii inalenga kuhakikisha waombaji wa ajira wanapata msaada kwa urahisi, haraka na kwa wakati, hivyo kuboresha uzoefu wao katika matumizi ya Ajira Portal.



# Livechat

## Namna ya kutumia Livechat




Ili kupata huduma ya livechat, muombaji anapaswa kufungua Ajira Portal kupitia simu au kompyuta.

Kubofya kitufe cha ujumbe kilichopo upande wa chini kulia wa ukurasa wa Ajira Portal.

Baada ya hapo, ataweza kujipatia msaada mwenyewe au kuwasiliana moja kwa moja na mtoa huduma wetu wa Dawati la Huduma kwa Wateja ili kupata ufumbuzi wa changamoto anayokutana nayo.

Huduma hii inalenga kuhakikisha waombaji wa ajira wanapata msaada kwa urahisi, haraka na kwa wakati, hivyo kuboresha uzoefu wao katika matumizi ya Ajira Portal.




## Namna ya kuondoa cheti au sifa iliyojazwa kimakosa

Iwapo muombaji ajira amejaza cheti au kiwango cha elimu (Academic Level) kimakosa na anahitaji taarifa hiyo iondolewe, anaweza kutuma ombi la kuondolewa kupitia mfumo kwa kufuata hatua hizi:

- Nenda sehemu ya Academic Qualifications;
- Chagua sehemu ya cheti husika kilichojazwa kimakosa
- Bofya kitufe cha “Request Removal

www.portal.ajira.go.tz




# Mchakato wa Ajira

Unaendeshwa kwa kuzingatia Haki, Uwazi na Usawa

Dawati la

# HUDUMA Kwa Mteja







## Dawati la Huduma kwa Wateja: Tuko Tayari Kukusaidia

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaendelea kuboresha huduma kwa waombaji wa ajira kupitia Dawati la Huduma kwa Wateja.

Iwapo una changamoto au unahitaji ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali ya ajira, unaweza kupiga simu na kuzungumza na watoa huduma wetu, ambao wako tayari kukusaidia kutatua changamoto yako au kukupatia majibu sahihi.

Usikae na changamoto peke yako, wasiliana nasi na upate msaada kwa wakati!

Website
www.ajira.go.tz

# ASANTE

## Mawasiliano



P.O.BOX 2320

0262160350

www.ajira.go.tz

Mtaa wa Mahakama,
Tambukareli, jijini Dodoma,
Tanzania

Sekretarieti ya Ajira Sekretarieti_ya_Ajira AjiraTV Ajirapsrs